



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA**



Kumb. Na. NDC/S.20/33/II/57

17/08/2023

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Newala anapenda kuwatangazia wataanzania wote nafasi za kazi kwa wenye sifa kutuma maombi:-

**MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III – NAFASI (2)**

**SIFA ZA MWOMBAJI:-**

- Awe amefaulu kidato cha nne (IV) au sita (VI)
- Awe amefuzu mafunzo ya Astashahada (cheti) “NTA Level 5” katika fani zifuatazo:-  
Utawala, Sheria, Elimu ya jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya jamii, au Sayansi ya jamii kutoka chuo chochote kinachotambulika na serikali.

**KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI**

- i. Kuwa katibu wa Halmashauri ya Kijiji;
- ii. Kuwa Mtendaji Mkuu wa Kijiji;
- iii. Kuwa mratibu wa utekelezaji wa sera na Sheria zilizotekelezwa na Halmashauri katika Kijiji;
- iv. Kuwa mshauri wa Halmashauri ya Kijiji kuhusu mipango ya maendeleo katika Kijiji;
- v. Kuwa msimamizi wa utekelezaji wa Sheria Ndogo pamoja na sheria nyingine zinazotumika katika Kijiji;
- vi. Kuwa mshauri wa Halmashauri ya Kijiji kuhusu masuala ya Ulinzi na Usalama;
- vii. Kuwa msimamizi wa utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na umaskini katika Kijiji;
- viii. Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote;
- ix. Kuandaa na kutunza rejesta ya wakazi wote wa Kijiji na
- x. Kuwajibika kwa Mtendaji wa Kata.

---

*Jengo la Utawala, Mtaa wa Mmovo Na. 75 Mitema Road 634338 Muungano, S.L.P 16, Newala, Simu Na :  
+255232410251, Nukushi : +25522410211, Barua pepe: [ded@newaladc.go.tz](mailto:ded@newaladc.go.tz), Tovuti: [www.newaladc.go.tz](http://www.newaladc.go.tz)*

## MSHAHARA

Cheo cha Mtendaji wa Kijiji daraja III kina Mshahara wa TGS B kwa mwezi.

### MASHARTI YA UJUMLA

- Mwombaji awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- Mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa.
- Mwombaji ambaye ni Mtumishi wa Umma apitishwe barua yake ya maombi kwa mwajiri wake.
- Mwombaji aambatanishe maelezo yake binafsi yanayojitosheleza (CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya Wadhamini (referees) watatu wa kuaminika pamoja na namba zao za simu.
- Maombi yote yaambatanishwe na nakala za vyeti vya elimu na taaluma kutoka vyuo vinavyotambuliwa na serikali.
- Testimonials, Provisional results, Statements of results n.k hazikubaliki.
- Waombaji waweke picha moja ya passport size katika barua zao za maombi.
- Waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vinafanyiwa ulinganishi na TCU na NACTE.
- Waombaji wote wanalazimika kuwa na namba ya utambulisho wa Uraia (National Identification Number) kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
- Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 31/08/2023 saa tisa na nusu alasiri.

Barua zote zitumwe kwa anwani;-

Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Newala,  
S. L. P 16,  
NEWALA.



Magreth V. Likonda

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA.**

**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**WILAYA YA NEWALA**

Jengo la Utawala, Mtaa wa Mmovo Na. 75 Mitema Road 634338 Muungano, S.L.P 16, Newala, Simu Na :  
+255232410251, Nukushi : +25522410211, Barua pepe: [ded@newaladc.go.tz](mailto:ded@newaladc.go.tz), Tovuti: [www.newaladc.go.tz](http://www.newaladc.go.tz)